# Kutimiliza Historia Simulizi:

## Kuwasaidia Wakristo Kusimulia Habari Zao

Jean Paul Wiest

## Kutimiliza Historia Simulizi: Kuwasaidia Wakristo Kusimulia Habari Zao

Kutimiliza Historia Simulizi ni warsha ya utendaji kazi inayodhamiriwa mahitaji ya watu wanaohitaji kutumia historia simulizi katika kuandika historia ya kanisa na misheni. Habari za mwili na damu za washiriki wakuu na mashahidi wa matukio muhimu na mipito katika habari za misheni inaifanya uandishi wa kihistoria kuwa wa kuvutia na yenye maana.

Kupitia kwa njia ya warsha ya mahojiano, kurekodi, na kuchuja data, washiriki wanajifunza namna ya kuzoa kumbukumbu zilizo hai kutoka kwa watu ambao wanahusika moja kwa moja—na kuziweka hai kumbukumbu za watu hao.

Washiriki kwenye warsha hii wanachukuliwa hatua moja moja katika njia za kuujenga mradi wa historia simulizi katika muktadha wa Ukristo. Kuanzia njia za kufanya mahojiano hadi mikakati, miradi iliyo sahili na changamano inawasilishwa.

Hii ni semina ya utendaji kazi. Kila wasilisho linafuatwa na kikao cha kufanya mazoezi. Kufanya kazi kwa vikundi vidogo vidogo kunawawezesha washiriki kujiamini na kupata kujua jinsi ya kuimarisha mradi wa historia simulizi.

Marejeleo Teule

Ives, Edward D. *The Tape Recorded Interview*. Knoxville, Tenn.: Univ. of Tennessee Press, 1995.
Ritchie, Donald. *Doing Oral History*. New York: Oxford University Press, 1993.

Dkt. Jean-Paul Wiest, ambaye alikuwa mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti na Elimu ya Misheni kilichoko Maryknoll kwa miaka ishirini, kwa hivi sasa anahudumu kama Mkurugenzi wa Utafiti katika Kituo cha Jesuit Beijing na pia profesa wa kuzuru wa Ukristo katika Chuo Kikuu cha Tsinghua kilichoko Beijing. Wiest alizaliwa Ufaransa na ana cheti cha Elimu Wakf wa Dini (*Sacred Theology Licentiate*) kutoka Chuo Kikuu cha Gregorian kilichoko Rome na shahada ya uzamifu( *doctorate*) katika historia ya Uchina kutoka Chuo Kikuu cha Washington huko Seattle. Huku utafiti wake ukimulika upande wa Umishonari wa Mkristo, Wiest ana tajriba ya nyanjani kule Ulaya na Asia.

# Mhadhara wa 1

## *Maelekeo ya Historia ya Mkristo Inayofungamana na Nyakati Zetu*

# Aina mbalimbali za Historia Kimapokeo

## Tarihi

Ni shajara ya matukio na jinsi ya kutokea kwake kiwakati kukiwa na kiwango kidogo cha, ama kutokuwepo kwa uhakiki.

## Historia za ndani

Zinaandikwa kwa minajili ya kuifanya jamii ijue asili yake na maendeleo.

## Historia Rasmi

Zina muhuri ya yule aliyeziidhinisha na aghalabu hurejelea kazi zinazodhamiriwa kutumiwa na watu.

## Historia Kariha

Zinanuiwa kuadilisha waumini na kuhamasisha watu kuitwa na Mungu kwa kazi fulani.

## Historia Ulimwengu

Huchukulia shani ya Ukristo kama tukio la kidini la upana wa kijamii na kiuchumi na lenye athari za kisiasa kutoka Magharibi dhidi ya nchi za Ulimwengu wa Tatu.

# Sifa za Historia ya Ushuhuda wa Mkristo inayofungamana na Nyakati Zetu

## Ni zaidi ya Historia Ulimwengu

Kuacha mambo muhimu ya kidini kama vile kustawishwa kwa Ufalme wa Mungu ama mwito wa kutoka kwa Mungu kwa kanisa kueneza Injili kutainyima Historia ya ushuhuda wa Mkristo kutoka kwa kipengele chake muhimu.

## Ala ya Kutathmini

Ikiwa hatutapata habari zilizohai kutoka kwa viongozi wetu na Wakristo wengine, habari muhimu kama vile kuanzishwa na maendeleo ya vuguvugu la kanisa katika janibu fulani zitatoweka watakapofariki.

## Huduma na Hatua kuelekea Ushirika

Historia ya ushuhuda wa Mkristo inapaswa kwenda sambamba na habari za wamishenari kama mwanzo na maendeleo ya vuguvugu la kanisa kama linavyoeleweka na kuhamasishwa na wenyeji.

## Kujenga Hiba ya Mapatano

Ikiwa mwanahistoria ni mtambajihadithi mahiri na mhakiki mpevu, taswira zake za wakati uliopita na ugawaji wake wa sifa na lawama utathaminiwa na wamishenari pamoja na makanisa ya kijadi kama kiwango kamili cha umoja wao kihistoria na ushirikiano.

# Mhadhara wa 2

## *Upangaji wa Mradi wa Historia Simulizi*

# Kubuni Mradi wa Historia Simulizi

Ili kuwa na mpango halisi na wa kutendekana, twahitaji:

1. Kujua kile tunachotaka kufikiliza.

2. Kujitayarisha vilivyo na kutilia maanani vitu vifuatavyo:

    - Mahali
    - Majina ya watakaohojiwa
    - Duru nyingine za habari
    - Muda
    - Hela
    - Kategoria/Maudhui/Mawazo
    - Hojaji

## MPANGO WA HISTORIA YA JAMII
## ORODHA YA MAELEZO

( MUHIMU: Herufi kubwa=Mada kuu
Habari nyingine=Mada ndogo

**MAPATANO:** Utajumuisha juhudi za wamishonari
Kukubali utamaduni mwingine, tabia ya nchi, n.k
(hali ya mhojiwa kujali ama kutojali
utamaduni na watu wa utamaduni huo.)
Utamaduni
Desturi
Matatizo
Lugha
Sakramenti
Kujali maslahi ya wengine
**KILIMO:**
Ushirika
Mazao
Jibini
Kutofaulu
Nafaka
Unyunyizaji
Mifugo
Fanaka
**TATHMINI:**
Ajenda
Kanisa Katoliki
Maryknoll
Njia za Misheni
Kazi ya Misheni
Binafsi
**SANAA YA UJENZI:**
Kanisa dogo
Kanisa
Ujenzi
Nyumba ya watawa
Mandhari ya Misheni
Vituo vya nje
Seminari
Shule
**MAJUKUMU:** (Tumia tu wakati
habari kabambe inapotolewa.Tazama pia **Daraka**)
Maendeleo (inahusisha afisi ya mwito wa Mungu)
Elimu/desturi
Eneo la Misheni(jina)
Parokia, n.k
Mawasiliano ya Kijamii
SSU (Kikosi maalum cha jamii)
Kikosi
**ASILI:**
Binafsi
Familia
**MAWASILIANO:**
Kila siku
Kidokezo
Barua
Gazeti
Jarida
Kitabu
Redio
Runinga
Malumbano
**DESTURI (**toa jina la desturi inayojadiliwa)
Ona pia **MAPATANO**
Ndoa ya zaidi ya mke mmoja
MAELEZO: (KUHUSU NANI kuorodheshwa, mahali
Picha
Nyumbani
Maisha
Familia
Parokia
Misheni
Mwenendo wa maisha
Mji
Kijiji
Jiji
Tukio
Kutawazwa
**ELIMU:** ( Kwa Wana-Maryknoll, mashemasi-utawa,
watu wasio mapadre, n.k)
Mafunzo ya kidini
Baada ya katekisimu; kwa minajili ya kufundisha ama
kutoa mafunzo kwa wengine. Ainisha kozi maalum kama mada ndogo ya 2
k.m. Elimu ya dini iliyo Huru
Shule ya Msingi
Sekondari (Shule ya Upili)
Chuo Kikuu (ndaki)
Uanajenzi
Masomo ya binafsi
Masomo ya Misheni
Mafunzo ya Misheni
Lugha
Ufundi
Sanaa ya uchoraji
Kituo cha watoto yatima
Shahada
Kutojua kusoma na kuandika
Mafunzo ya Uwajibikaji
Shule (chekechea hadi chuo kikuu)
Elimu ya kuendelea (k.m. CPE)
Kufundisha
**TATHMINI: (**Tazama **MPANGO)**
**UINJILISTI** (Kueneza imani. Inarejelea Ukatoliki pekee. Kwa madhehebu
mengine, tazama **DHEHEBU.**
Pia tazama **KAZI YA PAROKIA**.
Maono (Shauri ama elimu ya dini)
Njia (Kutembelea ama kujadiliana ana kwa ana n.k)
Mradi
Kubatilisha
Uanafunzi wa dini (inahusisha maagizo,ubatizo, n.k)
Mafunzo ya uongozi (wakatekista, n.k)
Mandhari ya mashambani
Tarakimu
**HELA:**
Umaskini
Utajiri
Parokia
Mshahara
Matatizo (na mashirika, n.k)
Mfumko
Mapato
Matumizi
Msaada
Mchango
Vyama vya mkopo
**JIOGRAFIA**
Tabia ya nchi
Mtetemeko wa ardhi
Umbo la ardhi
Mafuriko
Ukame
Kimbunga
Tufani
Ramani
**SERIKALI: (**tazama **SIASA**)
AFYA: (tazama pia **UTABIBU**)
Kuavya
Ulevi

Upangaji uzazi
Hitilafu kimaumbile
Upofu
Uchovu
Zahanati (mada ndogo 2 itakuwa Safari, kasha, n.k
Uziwi
Ugonjwa
Utumiaji mbaya madawa
Maambukizo
Kifo bila maumivu
Hospitali
Usafi
Jamii yenye ukoma
Hali za kuishi
Afya ya akili
Lishe
Kituo cha ulezi (kwa wazee)
Kichefuchefu
Upasuaji
Mafunzo
Kazi
**HISTORIA:**
Maryknoll
Jimbo
Dayosisi
Familia
Janibu(kikabila)
Binafsi
Kitaifa
Sanaa jadiiya
Misheni
Kuhusu (majina ya pili kutoa maelezo ama mtu maalum)
**ATHARI KWETU SIS**I: (Tazama pia **MAWASILIANO**)
Filamu
Maandishi
Nia
Siasa
Idara ya maendeleo
Janibu (kikabila)
Kitaifa
**MWINGILIANO KITAMADUNI: (**Itahusisha juhudi zote-
Hata juhudi za kimsingi za mwingliano wa kitamaduni-kwa kanisa na
Ujumbe wake katika kipengele cha utamaduni wa kila taifa na umri) tazama
Pia **MAWASILIANO**)
Ukopaji tamaduni
Tambiko
Ukristo
Ushirika Mtakatifu
Kuhusu
Sakramenti
Tafsiri
**UASILI**: Inarejelea kazi za wamisheni katika kuanzisha
wahudumu wa asili na wanadada, makatekista wenye mafunzo
kamili na utume. (tazama pia Mafunzo ya Uongozi chini ya
**UENEZAJI INJILI** na **KAZI YA PAROKIA)**
**SHERIA NA TARATIBU:**
Ujangili
Uhalifu
Kizuizini
Mashtaka
Mashindano ya kiukoo
Ukiukaji haki
Uharamia
Ghasia
Uasi
Hatua za kikatili
Uchunguzi
**MTINDO WA MAISHA:** (Tazama pia **MAELEZO**)
Kila siku
Jiji
Jamii (watu wanaoletwa pamoja kwa mujibu wa
uhusiano maalum, kama vile jamii kidini)
Mji
Kijiji
Anasa
Usasa
Chaguo la maskini
Kundi la kutoa msaada
**UTABIBU:** Kama kazi maalum (tazama pia **AFYA)**
**MALENGO**: (tazama pia **MPANGO**)
**KAZI YA PAROKIA** (hususan kuwalea Wakristo)
Maono (shauri ama Elimu ya dini)
Mandhari ya mashambani
Mandhari ya mjini
Mpango (ingiza kama mada ndogo 2:
Hatua ya Kikatoliki
Ch(Vy)ama vya vijana
Jeshi la Maria
Ndoa, n.k)
Ziara za nyumbani
Faraghani
Uinjilisti (Uanafunzi wa dini
kwa wasio Wakristo)
Maagizo (kwa wale tayari wamebatizwa)
Ushirika Mtakatifu (sakramenti, ziara, misa, n.k)
Maisha ya Mkristo
Usaidizi wa kijanibu
Ununuzi wa ardhi
Mafunzo ya ushemansi
Mafunzo ya uongozi (viongozi wa parokia, makatekisti, n.k)
Jamii za kimsingi
Vituo vya nje
Shule
Tarakimu
Sakramenti
Fanaka
Msisitizo
Kutegemea kwa
Kuanzisha parokia
**DHULMA:** Inarejelea udhalimu wa kidini. Kwa aina nyingine
tazama **SHERIA NA TARATIBU.**
Maandamano
Kizuizini
Kamata
Uufiaji dini
Vitisho
**MPANGO:**
Mazingira
Maono (shauri, dini ama ushauri wa dini)
Athari ya Vat.II
Utafiti
Dhamira (ya mbali, binfasi, Maryknoll, dunia, n.k)
Malengo
Wakurugenzi
Kufanyiza
Tathmini (tarakimu)
**SIASA: (** tazama pia **SERIKALI**)
Mkataba
Ukomunisti
Umaksi
Ukapitalisti
Usoshalisti
Uchukiaji wageni
Uzalendo
Matatizo
Maandamano
Kujihusisha
Kamata
Kizuizini
Mauaji

**UHUSIANO:** kutumiwa sambamba na orodha ya **KUHUSU NANI**. Kati ya (kuashiria "na") Pamoja na.

**KAZI YA KUTOA MSAADA:**
Chakula
Mavazi
Makazi
Shirika

**DINI:**

| | |
|---|---|
| Ukatoliki | Uprotestanti |
| Uislamu | Upentekosti |
| Ubuda | Tapo la Ekumeni |
| Kihindu/Kibanyani | Ukristo |
| Ujadi | Ustahifu |
| Imani za kijanibu | |

**MAJUKUMU:**

| | |
|---|---|
| Kazi | Utawala |
| Kufundisha | Afisi ya eneo |
| Kazi ya Parokia | Uinjilisti |
| Kikosi maalum cha jamii | Kanisa dogo (jela), hospitali ama vijana) |

**SWALI LA KIJAMII:**
Maswala ya kimaadili
Haki na amani
Ukandamwizaji
Kutojua kusoma na kuandika
Unyonyaji
Mradi wa jamii
Matatizo ya kifamilia
Vunjwa
Vuguvugu la haki za jamii
Uguriaji
Umaskini

**IMANI YA KIROHO:** (tazama pia **ELIMU**)
Faraghani
Mishonari
Tajriba ya kidini
Kiapo
Binafsi
Ustahifu

| **UCHUKUZI:** | njia ya usafirishaji |
|---|---|
| Mashua | Gari la moshi |
| Baiskeli | Ndege |
| Mguu | Basi |
| Pikipiki | Lori |
| Umma | Gari |
| Farasi | Punda |

**USAFIRI:**
Nyumbani (katika chi husika)
Ng'ambo (nje ya nchi husika)
Ajali
Matatizo
Usasa

**MAONO: (**tazama pia **MPANGO**)
Binafsi (kwa maono ya binafsi/mawazo kuhusu siku zijazo)

**MWITO WA KAZI:**
Upambanuzi (ikiwemo waso-mapadre)
Mishonari
Ukasisi
Yenye dini (Dada na Ndugu)
Usajilishwaji

**VITA**

| | | |
|---|---|---|
| VVI | VVII | Korea |
| Vietnam | Vita vya kieneo | (jina la vita, iwapo ipo) |

## Orodha ya mweleza Mpango wa Historia ya Jamii

**ORODHA YA KUHUSU NANI**

| | |
|---|---|
| Mwananchi wa asili | Mayatima |
| Atakaye | Wagonjwa |
| Watoto | Wagonjwa/akili |
| Mabuda/Sufi | Vyama vya Uzalendo |
| Mabuda/Watawa | Watu/Miji |
| Wafanyibiashara | Watu/Mashambani |
| Makatekisti | Wanafunzi wanaotaka kujiunga |
| Makatekisti/Wanawake | Makasisi/Wana-Maryknoll |
| Makatekisti/Wanaume | Waprotestanti |
| Makatekumeni | Wakimbizi |
| Makatekumeni/Wanawake | Wakristo wa melikora |
| Makatekumeni/Wanaume | Dada/Maryknoll |
| Watoto | Dada/ Wenyeji |
| Wakatoliki | Askari |
| Wakomunisti | Polisi |
| Shemasi | Wanafunzi |
| Madaktari/wa kigeni | Wanafunzi/Katoliki |
| Madaktari/wenyeji | Wakuu/Dini |
| Wafanyikazi/Mk1 | Walimu |
| Wahamiaji | Jeshi la Marekani |
| Wageni | Bikira |
| Wenye shamba | Wanawake |
| Maafisa wa serikali | Wanawake/Wamerikani |
| Wajaji | Wanawake/Wenyeji |
| Wachanga/wakifa | Vijana (umri mkubwa,balehe) |
| Wenye shamba | Vijana/kike |
| Wakristo wenye mashtaka | Vijana/kiume |
| Walimu wa dini | |
| Wamishonari wa kawaida | |
| Wenye ukoma | |
| Wenyeji | |
| Wana-Maryknoll | |
| Mabepari | |
| Wahamiaji | |
| Jeshi | |
| Wamishonari/Katoliki | |
| Wamishonari/Protestanti | |
| Waso-Wakristo | |
| Wanajenzi | |
| Wauguzi | |
| Maafisa | |

**MUHIMU:** Orodha hii ni mfano tu.Kundi lolote la kiisimu ama taifa linaweza kuingizwa. Kwa mfano, ikiwa mhojiwa anazungumzia Watu wa Mexico kwa jumla, "Wamexico" itajumuishwa. ikiwa anazungumzia kuwahusu Wahindi wa Maya huko Mexico "Maya" itakuwa uteuzi bora.

# KIOLEZO CHA HOJAJI

# NA MADA ZA

# MIRADI YENYE MALENGO MAPANA

# KIOLEZO CHA HOJAJI NA MADA ZA MIRADI YENYE MALENGO MAPANA

# MASWALI YA MAHOJIANO KWA WENYEJI

**I. Picha ya Mmisheni**

1. Ni nani hawa ama waliokuwa wamisheni wanaume na wanawake wa Maryknoll?

2. Mbona wapo ama walikuwa katika kijiji au jiji lako?

3. Ni nini walicho ama wanachojaribu kufanya?

4. Ni vipi wamefaulu ama walifaulu katika kile wanacho ama walichojaribu kufanya?

5. Walikuwa katika eneo lako kwa muda gani? Ni athari gani ama mabadiliko yapi waliyoyaleta maishani mwako na kwa kijiji ama janibu yako?

6. Maisha yao yalikuwa ama yako vipi?

7. Ni kwa kiwango gani wameweza kujitambulisha na maisha ya kijiji ama jiji lako?

8. Ni matatizo gani yaliyo ama yanayowakumba wakijaribu kuiga maisha kama yako?

9. Ni kwa kiwango gani walikuja kuwaelewa watu wako na maisha yako? Je, unaweza kukumbuka kisa ambapo walionyesha kuelewa ama kutoelewa?

10. Je, wanaume wa Maryknoll walikuwa na athari kwa wenyeji wanaume? Wanawake wa Maryknoll kwa wenyeji wanawake? Je wanaume na wanawake hawa walikuwa raia bora, wazazi bora, mume na wake bora kutokana na maingiliano hayo?

11. Ni kwa kiwango kipi mamishenari, hususan wale wa Maryknoll, ni ama walichangia katika mageuzi ya kisiasa?

12. Maafisa, Wakristi na watu wengine wanamaoni gani ama walikuwa na maoni ipi kuhusu Wana-Maryknoll? Maoni yako ni yapi kuwahusu?

**II. Uhusiano wa Wamisheni na wenyeji**

13. Ni kitu gani kilisababisha kukutana kwako mara ya kwanza na Wana-Maryknoll?

14. Uhusiano huu umekuwa vipi? [Ulishahibiana na uhusiano wa mwajiri na mwajiriwa? Walimu na wanafunzi?Wafadhili na mfadhiliwa? Wafanyikazi wenzako ama wenzako?Marafiki?Ama…?]* Je, ulihisi kama kwamba uhusiano huu ungelilipwa kwa namna hiyo hiyo?

    Je, uhusiano huo ulibadilika ama kutokeza katika miaka hiyo mfululizo?

15. Ni kwa njia gani kazi ya Wana-Maryknoll ilichangia katika ama kuathiri kazi yako ama jukumu lako katika kijiji ama jiji?

---

*Maswali yaliyo kwenye mabano yanapaswa kutumiwa tu kama kichocheo ikiwa mhojiwa atatatanishwa na swali la kijumla.

16. Ni kitu kipi ulichokifikiria ungelikitegemea kutoka kwa wamisheni? [ Kuongeza imani yako? Usaidizi wa kihela ama mali? Wosia wa masiala ya kijiji ama kijamii? Ushauri  kuhusu kazi ama biashara? Urafiki? Mengine?]

17. Je, ulihisi kama kwamba wana uwezo zaidi wa kimali, nguvu nyingi, hadhi zaidi ama hekima nyingi kukuzidi wewe? Kwa namna gani?

18. Je, ulihisi kama kwamba uhusiano wako na hawa wamisheni uliimarisha ama kudunisha uhusiano wako na marafikizo na majiranizo ambao si Wakristo? Je, uhusiano wako nao ulisababisha mabadiliko yoyote maishani mwako?

19. Uhusiano huu ulikuletea nini?[maadili mema ya kiroho? Mtazamo ulio mpevu wa mambo katika maisha? Hadhi zaidi?hela zaidi? Ile hali ya kujihisi kuwa na mamlaka na nguvu?mengine?]

20. Je, utapendekeza ama kuwaleta marafikizo ama jamaa zako katika uhusiano wa namna hiyo na wamisheni?

**III. Kuanzisha makanisa ya janibu**

21. Ni vipi hawa wamisheni walianzisha makanisa ya kijanibu? Nini kilichofanya kazi? Nini ambacho hakikufanya kazi?

22. Nani walikuwa wakristo? Walitoka katika hadhi zipi za kijamii na kiuchumi kwenye kijiji ama jiji lako? Je, ulikuwa Mkristo? Kwa nini? Ulipata mawasiliano na mafundisho kwa njia gani?

23. Ulipata mafunzo yapi kutoka kwa wamisheni kuhusu Mwenyezi Mungu? Kumhusu Yesu? Kulihusu Kanisa( Baba Mtakatifu, ubia wa Kanisa, Rome n.k)? Kuhusu maombi? Ni mabadiliko yapi mawazo yao yalisababisha kwa mintarafu ya maisha yako? Kwa uhusiano wako na wengine?

24. Maoni yako kuhusu mawazo hayo yamebadilika kwa kiwango gani katika miaka hii? Una maoni gani kuwahusu hivi leo?

25. Ni mawazo gani ambayo uliyapata yanavutia zaidi katika madhehebu ya  Kikristo?

26. Je, ulibatilisha kutoka dhehebu lisilo la Kikristo? Je, jambo hili lilisababisha mtafaruku kati yako na familia ama jamii yako?

27. Je, uhusiano wako na Wakristo wengine katika jamii ama kijiji chako ulichangia katika kubatilisha imani yako?

28. Je, ulikuwa kasisi? Mtawa?mbona? ulisajiliwa kivipi na mafundisho yalikuwaje? Jukumu lako katika kanisa lako la kijanibu lilikuwa  ni lipi na Wakristo? Na wale ambao sio Wakristo? Na Wamisheni wa kigeni?

29. Maisha ya Ukristo ulikuwa ni vipi katika parokia yako, ama ‘jamii yako ya msingi’?

30. Eleza majukumu yako katika parokia yako ama ‘jamii yako ya msingi’.

31. Je, unaweza kukumbuka baadhi ya watoa mafundisho wa kanisa katika eneo lako? Walikuwa ni akina nani? Ni vipi waliweza kuwa viongozi wa kanisa? Majukumu yao yalikuwa kwa namna gani?

32. Eleza jukumu la mkatekista. Waliteuliwa vipi na walifundishwa vipi?

33. Eleza uhusiano baina ya makatekista , watoa mafundisho wengine wa kanisa na wahubiri pamoja na wenyeji. Je, waliweza kusaidia kuwaelezea wamisheni kuhusu wenyeji ama wenyeji kuelezewa kuhusu wamisheni?

34. Je, ulitarajia kuwa mfundishaji wa kanisa? Je, ni jukumu ambalo watu katika jamii yako wangelipenda kulihimarisha?

**IV. Majukumu ya Misheni**

35. Eleza aina mbalimbali za kazi ambazo zilianzishwa na wamisheni wanaokaa mahali ulipoishi: kituo cha watoto yatima, zahanati, shule, kituo cha wazee, kambi ya wakimbizi, n.k.

36. Kazi hizi zilichangia kwa namna gani katika kuimarisha maisha ya wenyeji kijijini ama jijini?

37. Je, wewe ni kati ya 'wanajamii ya kimsingi?' ni jukumu lipi lililopewa wamisheni kwa mintarafu ya 'Jamii ya kimsingi?'

**V. Tathmini Jumla**

38. Ni mafundisho gani uliyoyapata kufuatia kuingiliana kwako na wamisheni?

39. Kwa maoni yako, ikiwa wamisheni wanataka kuleta Ukristo katika nchi yako, je, vijiji vidogovidogo ndivyo mahali kamili pa kuanzia, ama ilengwe jiji na viongozi wao? Je, yapo tofauti zozote?

40. Je, njia ipi ni tatuzi zaidi?[kuhubiri injili moja kwa moja? Kufadhili miradi? Kazi za Kielimu? Uwepo? Kuitikia na kuungama na maskini na wanaonyanyaswa?n.k.]

41. Unaelewaje matendo ya wamisheni wa Maryknoll hivi leo?

42. Je, unafikiria wamisheni wa Maryknoll wana nafasi siku za usoni kwenye kanisa katika nchi yako?kama ni hivyo, ni njia zipi unazopendekeza wao wazitumie? Ni mawaidha gani utakayotoa?

43. Unafikiria nini kuhusu jukumu la wamisheni wa kigeni katika nchi nyingine leo? Unafikiria wana jukumu la usoni katika kanisa la janibu?

44. Unafikiria taasisi ya dhehebu la Kikristo( yaani, Kanisa la Kirumi) ina nafasi katika hali ya baadaye ya nchi yako? Nchi na tamaduni nyingine?

45. Unafikiria ujume wa Kikristo na maadili inayowakilisha ina nafasi katika hali ya baadaye ya nchi yako? Katika nchi na tamaduni nyingine? Kama ni hivyo, ni nini kinachoweza kufanywa ili kisiwe 'dhehebu la kigeni'?

46. Je, uliweza kuyatoa maono yako kwa njia za hati ama katika machapisho yoyote yale?kama ni hivyo, yanaweza kupatikana wapi?

# MASWALI YA MAHOJIANO KWA WAMISHENI WA KIGENI

## I. Kujiandikisha kwa mmisheni, motisha na mafunzo

1. Ni sababu gani ilikufanya ukajiunga na Shirika na kazi ya misheni? Kwa nini ulienda katika eneo ama kikosi chako?

2. Elimu yako na desturi yako ilikuwa ni vipi kabla ya kwenda ng'ambo? Elimu na desturi ipi ulipata kutoka eneo lako? Ni kiwango gani cha lugha na tamaduni?je, uliweza kusoma na kuandika katika lugha za kienyeji?kwa weledi? lahaja gani?

3. Ni nini( kwa maoni yako) ilikuwa motisha kuu kwa Wana-Maryknoll? [kubadilisha nyoyo? Kuwasaidia wenye mahitaji? Kushirikisha utamaduni na dhehebu uliobobea wa Marekani? Mengine]*

4. Maono na malengo yako ya awali ya kazi yako ya Maryknoll katika eneo ama idara yako yalikuwa yapi kabla ufike mahala hapo? Je, maono na malengo hayo yalibadilika?

5. Eleza tajriba yako na waasisi wa Maryknoll. Unafikiria taathira ipi iliyoko kutoka kwa waasisi hawa kwa jamii?kwako je?

6. Ni nani waliyokuwa na athari kubwa zaidi kwako wewe wakati wa kupata mafundisho yako kule Marekani? Kwa nini?

## II. Maisha na tajriba ya Makasisi na Ndugu katika maeneo ama vikosi vyao

7. Unaamini kuwa malengo makuu ya kazi ya Maryknoll katika eneo ama idara yako ni yapi? Unaamini kuwa ni masiala gani yaliyo makuu, mivutano, matatizo na maamuzi ambayo Maryknoll inapaswa kuyatekeleza katika eneo ama kikosi chako?

8. Ni miradi ipi ilikuwa ama inayotia fora katika kazi ya Maryknoll katika eneo ama kikosi chako? Gani haikutia fora?

9. Ni kazi zipi zilizokuwa ama zilizo rasmi za makasisi wa Maryknoll? Ni kazi zipi zilikuwa ama zilizo rasmi wa ndugu wa Maryknoll? Kazi hii ya makasisi na ndugu ziliingiliana ama zinaingiliana vipi na ile ya watawa?

10. Eleza maisha ya kila siku na kazi, ratiba ya kila siku ya a) Makasisi, na b) Ndugu

11. Ni kwa namna gani maisha na kazi ya makasisi na ndugu ilibadilika na kuendelea katika miaka hiyo?

12. Jukumu la kimsingi la Maryknoll lilikuwa ni kueneza injili na kujenga makanisa.Ni njia zipi zilizotumika? Zipi zilizofaulu? Zipi hazikufaulu? Ni mabadiliko yapi yaliyotokea tangu Vatican II? Je, jukumu la Maryknoll ni tofauti leo?. Kama ni ndiyo, kwa namna gani na kwa nini?

13. Ni funzo gani Maryknoll lilipata kufuatia tajriba ya eneo ama kikosi chako?

14. Je, ni mambo gani yaliyokutosheleza na kukukidhi katika tajriba yako ya kikazi? Yapi yalikuwa magumu zaidi?

15. Uhusiano wako na mashirika mengine ya kidini ( Katoliki na Kiprotestanti) ulikuwa vipi? Na madhehebu ya kitamaduni?

---

*Maswali yaliyo kwenye mabano yanapaswa kutumiwa tu kama kichocheo ikiwa mhojiwa atatatanishwa na swali la kijumla.

**III. Kanisa la janibu**

16. Eleza usajili, mafunzo na kazi ya makasisi na watawa walioko chini ya utawala wa Maryknoll. Eleza kuhusu wenzako. Uhusiano wako nao ulikuwa ama ni upi? Wanafanya ama walifanya nini? Je walikuwa ama wanayo nyadhifa zilizo na mamlaka ama majukumu?

17. Ukifanya kazi kwenye mandhari ya parokia, eleza maisha ya Kikristo ya parokia yako (ushirika mtakatifu, mafunzo ya katekisimu, n.k.) Eleza kazi ya kipekee ya kituo chako cha misheni.

18. Eleza majukumu ya makatekista (wake kwa waume). Ni kwa njia gani waliteuliwa ama wanateuliwa na kupewa mafunzo? Wanalipwa vipi? Ni aina gani ya mafunzo ya ukatekisimu wanazo ama walizozitoa? Eleza majukumu ya makatekista wanawake? Kulikuwa ama kupo wenyeji walioajiriwa na Maryknoll? Walifanya ama wanafanya nini?

19. Eleza uteuzi, mafunzo na kazi ya viongozi wengine wa kanisa.

20. Eleza kazi ya kituo chako cha misheni kama vile vituo vya watoto yatima, shule, kazi za utabibu na huduma kwa jamii. Ni kwa njia gani hili lilichangia katika kutekeleza malengo ya kimsingi ya Maryknoll katika eneo ama kikosi chako?

21. Ukifanya kazi katika mandhari ambayo sio ya parokia, eleza kazi yako, majukumu yako na uhusiano wako na wenyeji. Ni sifa zipi unazozianisha na kule kujihusisha na wenyeji hao?

22. Je, una mawasiliano na jamii za kimsingi za wakristo ama makundi yanayochipuka ya kidini katika eneo ama kikosi chako?kama ni hivyo, eleza.

23. Ni mmisheni yupi wa Maryknoll unayempenda zaidi?kwa nini? Ni nani kwa mujibu wako ambaye ndiye mmisheni shupavu kabisa katika eneo ama idara yako? (sio lazima awe ni Mwana-Maryknoll.)

**IV. Uhusiano na wenyeji, siasa na jamii**

24. Unahisi kuwa ume/ulikuwa na uhusiano wa karibu na wenyeji? Uliielewa jamii yao na utamaduni wao vema?

25. Wewe (ama wengine) wanakumbana na uhasama dhidi ya wageni: kauli za kuikashifu Marekani? Eleza visa hivi. Je, kuna kitu ambacho ungependa kiangaliwe kama ‘ Utawala wa kiutamaduni?’

26. Uli/unapata uzoefu fulani kuhusu mivutano ya kijamii na kiuchumi pamoja na kisiasa inayo/iliyofanyika katika eneo ama kikosi chako? Kabla ya kutoka? Nyanjani? Maoni yako ni/yalikuwa yapi kuhusu mivutano hiyo? Unaelewa vipi hali iliyoko ya kisiasa na kijamii? Ni magazeti na majarida gani una/ulisoma? Ni wapi kwingine unapata habari?

27. Je, ume/ulikuwa na tajriba ya kibinafsi na ghasia za kijamii, bajangili, n.k?

28. Ni uhusiano upi ulioko ama ulipo na marafiki na wafanyikazi wenzako ambao ni wenyeji wa eneo ama kikosi chako? Uli/unawatembelea majumbani mwao, kula chakula nao na wao kufanya hivyo kwako? Je, una/ulikuwa na marafiki wa karibu miongoni mwao?

**V. Athari ya Maryknoll kwa maoni ya Marekani kuhusu eneo ama kikosi**

29. Je, uliandika kuhusu tajriba yako? Maandishi haya yanapatikana?

30. Vipi wewe una/uliathiri pamoja na wana-Maryknoll wengine maoni ya Marekani dhidi ya eneo ama kikosi chako? Toa mifano.

# Mhadhara wa 3

## *Kabla Mahojiano na Mahojiano*

# MRADI WA HISTORIA SIMULIZI
## ORODHA YA YATAKAYOHOJIWA

1. Wasiliana na msimulizi, na kuhakikisha kuwa anauelewa mradi barabara.

2. Ni vema kupata ufahamu wa hali wa mambo ya kimsingi kumhusu msimulizi

3. Ikiwezekana, panga ziara kabla ya mahojiano ili wewe na mhojiwa mfahamiane.

4. Tayarisha orodha ya hoja zitakazojadiliwa.

5. Piga msasa vyombo vya kazi kabla mahojiano. Mahojiano hayapaswi kuwa kikao cha kupata mafunzo mtu akiwa kazini.

6. Hakikisha una kila kitu kinachohitajika kabla ya kuondoka kwenda kwa mahojiano: Rekoda, maikirofoni, adapta, batari mpya, kanda, penseli, karatasi, na fomu za kuidhinisha.

7. Hakikisha unafanya mahojiano ndani ya chumba ambacho kitapunguza kelele za nje.

8. Hakikisha kuwa rekoda inarekodi. Jitambulishe, msimulizi, tarehe, mahali, sababu ya mradi huo, na muulize msimulizi kukubaliana na mradi.

9. Mahojiano. Wakati wa mahojiano, andika nomino za mahali na watu na pia maneno mengine ambayo hijahi zao zinatiliwa shaka.

10. Hakikisha unamuuliza msimulizi kuhusu hijahi na maswali mengine ambayo unaweza kuwa nayo kuhusu mahojiano.

11. Hakikisha msimulizi anatia sahihi fomu za idhini.

12. Unapofika nyumbani ama afisini, andika chini mambo muhimu yalitokea wakati wa mahojiano ambayo yanaweza kuwafaida wenye kuandika fahirisi na kunakili.

13. Tuma barua ya “mkate na siagi” kumshukuru msimulizi.

Imetoholewa kutoka *Talking about Connecticut: Oral History in the Nutmeg State.*

# NJIA YA KUFANYA MAHOJIANO

## ALA

- Mashine ya kanda
- Kanda
- Batari
- Vifaa vya kunasa
- Kalamu kadha
- Daftari

## ALAMA

- Hakikisha zile kanda zimewekwa alama vizuri unapozitumia

## MAHOJIANO HASWA

- Anza na mazungumzo ‘yasiyo rasmi’
- Usibishane na mhojiwa
- Tumia maswali kukuongoza tu
- Tumia uwezo wako wa kusikiliza
- Maswali mengine magumu zaidi yanapaswa kuja mwishonimwishoni

## WAKATI WA MAHOJIANO

- Isipite dakika 90 kwa kila kikao

## ONDOKA KWA HESHIMA

# MIONGOZO: KUFANYA MAHOJIANO KWA UZURI

## **MAMBO YA KUEPUKWA**

**X** Kulazimisha imani na mawazo yako kwa mhojiwa

**X** Kutaka jawabu kwa maswali ambayo ni nyeti

**X** Kuuliza maswali ambayo yanamwongoza mhojiwa

**X** Kuipa rekoda kipaumbele

**X** Kufanya makelele mengi

**X** Kubishana na mhojiwa

**X** Kufanya mahojiano kuwa marefu kiasi cha kukuchosha na mhojiwa

| Maswali Wazi na yale Funge | |
|---|---|
| **Maswali Funge** | **Maswali Wazi ama Amsha** |
| Ulizaliwa wapi? | Nini unachokumbuka kuhusu mahali ulipozaliwa? |
| Wazazi wako walizaliwa wapi? | Wazazi wako walikuambia nini kuhusu maisha yao? |
| Je familia yako ilikuwa na hafla? | Eleza hafla ya familia yenu. |
| Likizo zipi ambazo familia yako walikuwa wakisherehekea? | Familia yako walisherehekea likizo kivipi? |
| Je, dini ilikuwa muhimu kwa familia yako? | Niambie kuhusu hali ya kidini ya familia yako. |
| Ulimaliza shule lini? | Shule yako rasmi iliisha kwa namna gani? |
| Je, wewe na marafiki zako walicheza kama watoto? | Eleza baadhi ya michezo uliyocheza kama mtoto. |
| Je, ulishiriki katika Vita vikuu vya II vya Dunia? | Nieleze kuhusu maisha yako wakati wa Vita Vikuu vya II vya Dunia. |
| Je, ulipata kazi baada ya vita? | Niambie ulichokifanya baada ya kutumikia vitani. |
| Je, uliipenda kazi yako? | Eleza jinsi ulivyohisi katika kazi yako. |

| Mifano ya Maswali ya kumwongoza Mhojiwa | |
|---|---|
| **Ya kuongoza** | **Yasiyofungamana na upande wowote** |
| Bila shaka ulifurahi sana usiku wa uchaguzi. | Ulihisi vipi usiku ule wa uchaguzi? |
| Haukumpenda Bw. X.Ulimpenda? | Niambie kumhusu Bw. X. |
| Utasema nini kuhusu tabia ya kuchukiza ya Bwana Jones? | Bwana Jones alifanya nini siku hiyo? |

**Usifanye Hili!**

*Huu ni uteuzi kutoka kwa mahojiano ya kaimu kasisi mmoja wa Maryknoll ambaye alifanya nyingi ya kazi yake ya umisheni huko Peru. Sasa hivi anaongoza parokia yake Marekani na ametoa idhini yake kwetu sisi kuitumia kama mfano darasani.*

**Mhojiwa:** Nilikuwa nikifikiri kuwa litakuwa ajabu kutia saini makubaliano kwa mara nyingine (akicheka), kama walivyokuwa wakifanya leo. Nimefurahikupita kiasi kwamba walikuwa wanane kutoka dayosisi nane za nchi, ikiwemo Anchorage, Alaska! Hakika, inapata usaidizi kutoka kwa Maaskofu wa nchi. Naamini Maryknoll ilikuwa na sherehe za kutawazwa makasisi takriban nane mwaka huu, lakini wana makaimu wanane. Kwa hivyo nalona hilo kama hatua nzuri, na nilikuwa nikiwaambia adhuhuri ya leo. Hiyo ndiyo mojawapo ya sababu niko hapa kwenu na nilipaswa kuwaelezeni tajriba yangu. Ni kati ya matukio muhimu sana maishani mwangu kama kasisi, kuja katika Maryknoll, kuwa na maono ya dunia, kuweza kujifunza lugha mpya na utamadumi mpya, kwenda katika nchi nyingine. Hiyo imetoa kipengele kingine katika ukasisi wangu, na nina hakika itakuwa hivyo kwa hawa wengine wanane wanaokuja. Kwa hivyo, nauona mradi kama ni muhimu sana kama kipengele muhimu kwa utume wa Maryknoll ulimwenguni, na ninafikiria inaimarisha kazi kwenye dayosisi. Ni kweli kuwa Maryknoll iliasisiwa, naam, na makasisi wawili wa dayosisi.

**Mhoji:** Kuwakilisha Kanisa Marekani, hususan wahubiri wa dayosisi

**Mhojiwa:** Kwa hivyo nafikiri ni ajabu. Hakika ilikuwa ajabu wakati wa maisha yangu (akicheka), na baada ya kuhudumia kwa miaka sita kwa mara ya kwanza Peru, na kisha miaka mitano hapa Maryknoll, New York katika vyeo mbalimbali kwenye kituo cha Haki na Amani. Nilimuuliza Askofu, wakati miaka yangu sita ilikuwa ikiisha katika parokia niliyokuwa nikiishi, ruhusa ya kurejea. Naye hakuwa huru kuniacha miye niende, lakini nafikiria kuwa ni mradi shani, na bila shaka ningependa kuona kuwa inakuwa na kuendelea. Na hoja kuwa wako wanane, ni..

**Mhoji:** Namjua James Anthony Walsh, ndiyo, alikuwa akiitembelea Maryknoll pale Los Altos katika safari zake za mashariki. Alizuru mara kwa mara Mashariki na angepumzika, angepaa na kurudi, na kutupa sisi ripoti. Kila mara atatoa taarifa kuhusu aliyoyaona Mashariki, na hakika atazungumza, na alikuwa wa kuwapa watu msukumo. Lakini Wana-Maryknoll wa awali vilevile walikuwa na moyo, na tuliwajua watu hao hata zaidi.

Kwa hivyo, sasa nina hamu ya kukusanya vitu hivi kama walivyofanya waasisi. James Antony Walsh alikuwa shupavu katika historia, na aliweza kuandika na kuwasiliana kwingi, na alikuwa anapendezwa sana na somo hilo. Na nina shauku kuhusu hii kazi.

**Mhojiwa:** Kwa hivyo unaiweka historia ya eneo la Bolivia kwa pamoja?

**Mhoji:** Ndiyo, ndiyo, eneo lote la Bolivia.Tulienda pale mnamo ’42, na tumeanzisha mambo mengi ambayo yamekuwa. Kama vile zahanati ndogo zilikuwa hospitali kubwa, shule ya vyumba viwili imekuwa shule kuu, ya sekondari na advansi. Na tulianzisha mashirika, hakika tulianzisha vuguvugu hili. Tuliwasaidia makasisi kutoka dayosisi nyingi kuanza kazi zao. Watakatifu Louis, Lacrosse, Dubugue, hakika, idadi yao kamili sijui, lakini walionyesha nia yao angalau, na wengi wao walichangia vizuri. Ushirika wa Mtakatifu James ulipata msukumo kutoka kwa Wana-Maryknoller wa Bolivia, na Nuncio walitaka kujaribu kuwapata makasisi, Wana-Maryknoll huku wakiwa wanasita kidogo, kwa sababu walifikiri Maaskofu watalalamika, lakini kwa kweli (akicheka) hawakufanya hivyo! Hakika, walilipinga wazo hilo kwa kuhofia kuwa lingekwenda kinyume na kazi ya Maryknoll, lakini baadaye walikaribia.,

Nilijua ingenifurahisha kwa sababu Ed Fedders alikuwa amenizungumzia kuhusu uwezekano wa kupokea katika shule ya lugha, ambapo nilikuwa mkurugenzi ’55, ’56, ’57. Kwa hivyo nilikubali kupata moja, sikuona ugumu , lakini kulikuwa na hili tatizo la Maryknoll.

**Mhojiwa:** Ah, mara hiyo?

**Mhoji:** Ndiyo, naam, ona ilikuwa inakuja kutokea….

MWISHO WA KANDA
MWISHO WA MAHOJIANO

## A. Mkataba wa Mhoji

Ukanda huu (ama kanda hizi) na nakili zinazoambatanishwa ni matokeo ya moja au zaidi ya mahojiano ya kujitolea yaliyofanywa na__________________________________pamoja na_________________________

Msomaji yeyote wa nakili anapaswa kuzingatia akilini kwamba yeye anasoma nakili ya mazungumzo yetu, na kwamba ukanda, sio nakili, ndiyo stakabadhi ya kimsingi.

Nauruhusu Mradi wa Historia wa Ushirika wa Maryknoll na watafiti wote waliyoidhinishwa ama wanaohusishwa na Mradi wa Ushirika wa Historia matumizi yote iwapo mahojiano haya na matumizi yote ya vifaa vingine ambavyo navitoa kwa Mradi.

___________________________ ____________________________________

Sahihi ya Mhoji Tarehe

___________________________ _____________________________________

Sahihi ya Mhojiwa Tarehe

## B. Mkataba wa Mhoji

Tarehe:________________________________

Mimi,_________________________________, natoa idhini kwa maojiano yangu na_________________________________ kutumiwa na watu binafsi wanaojihusisha na uandishi wa Historia ya Jamii ya Misheni ya Maryknoll huko Brazil. Natoa idhini zaidi kwa vifaa hivi kutolewa kwa Mradi wa Historia ya Jamii ya Maryknoll wa Kituo cha Utafiti na Elimu ya Misheni na kumbukumbu za Maryknoll ili fikira na mawazo yangu yapatikane kwa watafiti wa usoni.

________________________________ _______________________________

Sahihi ya Mtahiniwa Tarehe

## C. Mkataba wa Mahojiwa

(Kutumiwa tu kunapotokea hali ya masharti)

Mimi,________________________________, natoa michango ifuatayo kwa Mradi wa Ushirika wa Maryknoll, na kupitia kwake, kwa Kumbukumbu za Misheni ya Maryknoll, na ningependa kuweka masharti yafuatayo kwenye vifaa vya mahojiano:

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

______________________________ ____________________________________

Sahihi ya Mhojiwa Tarehe

### Shukrani

Mradi wa Kihistoria wa Ushirika wa Maryknoll unatoa shukrani za dhati kwa michango hiyo juu kwa Mradi.

______________________________ ____________________________________

Sahihi ya Mkurugenzi wa Utafiti Tarehe

# Mhadhara wa 4

# *Nakili*

# NAKILI

- Weka alama kwa kanda yako
- Kila kanda ya kaseti inapaswa kuwekwa alama dhahiri
  - -Juu ya kanda ama kisanduku cha kuweka kanda
- Weka orodha ya hijai sahihi
- Panga alama za muundo
- Kuwa yakini na tarehe za kumaliza kazi
- Jadili gharama kabla ya kuanza
- Tumia wino nyekundu kuhariri nakili
- Fanya tathmini ama hariri kila mahojiano

# ALAMA ZA MAHOJIANO

| | | |
|---|---|---|
| Kasisi John Q. | | 01/01/93<br>Mahojiano A |
| | **SMITH** | |
| Katika kituo cha Maryknoll | | Kanda 1 juu ya 3 |

Mahojiano ya Kasisi John Q. Smith na Jane Jones katika kituo cha Maryknoll

Kanda 1 juu ya 3, 01/01/93

Annel: Ndiyo, hayo ndiyo ya pekee unayoweza kuyafanya. Nina furaha kuwa ~~kuwa~~ Wanadada wa Maryknoll ~~tuna~~ wana sera kuwa, uwe nani,uwe mkuu jinsi gani na umetukuka jinsi gani,unaweza kufanya kazi ya kiwango cha chini kwa muda. Ikiwa ningelitaka kuja huku na kufanya kazi kama daktari hapa, labda wangeniweka katika orofa ya nne, kufanya kazi ~~tabibu~~ na watabibu wetu, ama kitu kama hicho.

Nilitaka kuliruka jukumu hilo kwa muda na lilikuwa fursa nzuri kwangu. Nilikuwa nimeitwa kwa muda mrefu. Nasema kwamba, mbali na kufanya kazi yote ya kufundisha, nilikuwa vilevile nimefanya kazi nyingi hospitalini na mambo ~~mengi~~ mengine zaidi. Na ninafikiria sikutaka kila mara kuitikia mwito wa magonjwa ya watu. Ilichangamsha. Lakini kwa sasa niko tayari kabisa kurudi tena katika udaktari na kuwahudumia wagonjwa.

McDonald: Kwa hivyo, umekuwa nje tangu 1988?

Annel: Ndiyo, mwishoni mwa 1988, miaka ~~minane~~ minne.

McDonald: Na ujafanya kazi yoyote ya ~~matabibu~~ matibabu tangu wakati huo?

Annel: Hapana, hapana kwa hakika. Sio moja kwa moja mbali na kuzungumza kuhusu kwayo na kufundisha. Kilichokaribiana na matibabu kilikuwa ni kwamba wakati huu wote nilikuwa hapa Marekani, nimekuwa nikifanya kile kinachojulikana kama mafunzo ya kozi za ugeuzaji.

McDonald: Sijapata kuisikia

Annel: Inajikita katika njia za Pablo ~~Fraile [?]~~ Freire ya elimu utendaji, na kuwapa watu majukumu ya kupata elimu. Na nimetoa mafunzo ya kozi hizo.Sio utabibu haswa, lakini inakaribiana na kile nilichokifanya na wafanyikazi wa afya, na aina ya (nafasi) njia za mafunzo tulizozitumia.

McDonald: Ninafikiria nitakuchukua had wakati uliopo sasa.

Annel: Sawa. Hutaki kujua zaidi kuhusu hospitali iliyoko ~~Jakotenanga~~ Jacaltenango na kazi ile ya afya?

McDonald: Iwapo tutakuwa na wakati, ningelipenda niyajue zaidi kuhusu hayo. Ndiyo,ningelipenda kujua hayo zaidi (akicheka), lakini pia ningelipenda kujua kuhusu huduma hii ya UKIMWI. Je, utakuwa unaenda kufanya hilo namna ulivyofanya mafunzo?

Annel: Ninafikiria kila kitu nilichokifanya na nina nuia kukifanya hadi sasa ni kuhusu mafunzo ya huduma ya ~~UKIWI~~ UKIMWI. Na sisi huileta historia yetu pamoja nasi ninafikiria. Ninahisi Mungu amekuwa akinielekeza katika hili.

Kwa mwaka mmoja na nusu uliopita, nilihisi nimeitwa kwa maombi kuiambia jamii yangu kwamba huku ningali kijana mdogo wa kuujua utamaduni na lugha nyingine, nitakuwa radhi ~~kufanya hivyo~~ kubadilisha maeneo iwapo yatakuwa tayari

# Mhadhara wa 5

## *Uhakiki wa Kimaudhui*

# UHAKIKI WA KIMAUDHUI

ni uainishaji wa data yako kutoka mahojiano yako kwa mujibu wa mfumo unaoambatana na mahitaji yako na lengo lako na unaofaa kabisa kwa kadiri ya bajeti na kuwepo kwa vifaa vyako.

**Mahali palipojadiliwa** **Vika/Dayosisi** **Parokia/Taasisi**

---

| *Mada Kuu* | *Mada ndogo* | *Mada ndogo 2* | *Kumhusu nan* | *Miaka-Kutoka/hadi* | *S* | *O* | *C* | *PG* | *#PGS* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |

**RIPOTI BINAFSI YA: ROBERT E. LEE**

| MADA KUU | MADA NDOGO1 | MADA NDOGO 2 | KUMHUSU NANI | MIAKA KUTOKA | HADI | S | O | C | PAG | PGS | ALAMA | MAHALA | VIKA/DAYO | PAROKIA/TAASISI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KILIMO | MAZAO | UBANI | | 1943 | | | | C | 6 | 1 | A | MEXICO | YUCATAN | |
| SANAA/UJENZI | UJENZI | POLE/YA KANISA | VERHAGEN,NORBERT | 1948 | | S | | | 7 | 2 | A | MEXICO | MJI MKUU MEXICO | ARINAL |
| MAELEZO | PICHA | YA | MORRISON,JOHN | | | | | | 22 | 1 | A | MEXICO | | |
| MAELEZO | PICHA | YA | WALSH,JAMES E | | | | | | 21 | 2 | A | MEXICO | | |
| MAELEZO | PICHA | YA CARILLO PUERTO | | 1943 | 1944 | | | | 24 | 2 | A | MEXICO | QUINTANA ROO | CARILLO PUERTO |
| MAELEZO | PICHA | YA MJI WA MEXICO | | 1938 | | | | | 23 | 2 | A | MEXICO | MJI MKUU MEXICO | CARILLO PUERTO |
| MAELEZO | MJI | JINA LABADILIKA | | 1943 | | | | | 5 | 2 | A | MEXICO | | |
| ELIMU | SEMINARI | MAISHA | LEE,ROBERT E | 1939 | 1949 | | | | 3 | 1 | A | MAREKANI | | |
| UINJILISTI | YA | | VIJANA | 1989 | | | | | 11 | 2 | A | MEXICO | | |
| UINJILISTI | KAZI YA PAROKIA | KUBADILI | WANA-MARYKNOLL | 1943 | 1989 | | O | C | 18 | 2 | A | MEXICO | | |
| JIOGRAFIA | TABIA YA NCHI | JOTO/CHEPECHEPE | | 1943 | | | | C | 5 | 1 | A | MEXICO | YUCATAN | |
| JIOGRAFIA | MTETEMEKO WA ARDHI | | LEE,ROBERT E | 1985 | | | | | 23 | 2 | A | MEXICO | | |
| AFYA | UGONJWA | SARATANI,MOYO,N.K | LEE,ROBERT E | 1970 | | | | | 14 | 3 | A | MEXICO | MJI MKUU MEXICO | |
| HISTORIA | BINAFSI | & FAMILIA | LEE,ROBERT E | | | | | | 1 | 2 | A | MAREKANI | BROOKLYN | |
| MTINDO WA MAISHA | | YA | WANA-MARYKNOLL | 1943 | 1989 | | | C | 25 | 2 | A | MEXICO | QUINTANA ROO | CARILLO PUERTO |
| DHULMA | VITISHO | NA JESHI LA MEXICO | WANA-MARYKNOLL | 1943 | | | | C | 6 | 3 | A | MEXICO | YUCATAN | |
| DHULMA | VITISHO | NA JESHI LA MEXICO | WANA-MARYKNOLL | 1948 | | | | | 24 | 1 | A | MEXICO | | |
| UHUSIANO | KATI YA | WAMISHENI WASAIDIZI & MAKASISI/MARYKNO | | 1989 | | | | | 17 | 2 | A | MEXICO | | |
| UHUSIANO | KATI YA | WASEMINARI | LEE,ROBERT | 1939 | 1943 | | | | 3 | 2 | A | MAREKANI | | |
| UCHUKUZI | FARASI | | LEE,ROBERT | 1943 | 1944 | | | C | 25 | 2 | A | MEXICO | QUITANA ROO | CARILLO PUERTO |
| KAZI | UFAHAMU | | LEE,ROBERT | 1932 | 1937 | | | | 1 | 2 | A | MAREKANI | BROOKLYN | |
| VITA | VVII | | | 1948 | | S | | | 7 | 2 | A | MEXICO | YUCATAN | |

# Mhadhara wa 6

## *Mapitio na Mapendekezo ya Kuandika*

## MAPITIO 1: Kabla ya mahojiano

1. Zingatia tangu mwanzoni mwa mradi kadiri ya watumizi.

2. Pata uzoefu wa yaliyoandikwa katika somo hilo.

3. Upeo wa mradi wako unapaswa kwenda sambamba na idadi ya mahojiano ambayo unaweza kuistahimili kutoka utafiti hadi unapoishughulikia.

4. Fanya utafiti kwa kina mtu binafsi na yale yote unayonuia kuikamilisha wakati wa mahojiano.

5. Kila mara yatathmini mahojiano yako na fanya kazi kuimarisha njia zako za mahojiano.

# MAPITIO 2: Mahojiano yenyewe

1. Kila mara sikiza kile mhojiwa anachokisema.

2. Kuwa tayari kufuatilia habari zisizotarajiwa zilizotoka kwa mhojiwa.

3. Usichelee kukubali kuwa haukufahamu kitu na uliza uwekewe wazi.

4. Usikuwe na kikao kimoja pekee cha mahojiano ila tu kama kwa maoni yako mhojiwa ametoa habari tosha kuhusu mada.

# MAPITIO 3: Baada ya mahojiano

1. Anza kuishughulikia mahojiano punde tu unapomaliza.

2. Nakili kila inapowezekana.

3. Watambue mhojiwa na mhoji mwanzoni mwa kila nakili na hakikisha kila mmoja wao anatia sahihi hati ya zawadi, masharti maalum yakielezwa kwa weledi ni wakati gani mahojiano yanaweza yakafanyiwa utafiti na wengine.

4. Tengeneza fahirisi ya nakili.

5. Zihifadhi kanda katika hali ambapo pima ya joto na uchepechepe zinabakia katika vipimo vinavyotakikana.

6. Tangaza kwa masafa marefu kuwepo kwa mahojiano yako.